



23 Machi, 2017

### **TUJIPANGE KUZIBA PENGO LA MADAKTARI NCHINI KWANZA**

Kwa mujibu wa maelekezo ya Shirika la Afya Duniani (WHO) katika nchi zinazoendelea kama Tanzania, inashauriwa daktari mmoja ahudumie watu wasiozidi 8,000. Kwa kuwa Tanzania inakadiriwa kuwa na watu takribani milioni 50, basi tulitakiwa tuwe na madaktari 6,250 wanaotoa huduma hospitalini.

Tamko la serikali la tarehe 21 Machi 2017 limesema madaktari wanaotoa huduma Tanzania ni 2,790. Hii ina maana kwamba tuna pengo la madaktari 3,460 sawa na asilimia 55.4 katika hospitali zetu nchi nzima.

Pamoja na pengo hilo, hivi karibuni serikali ya Tanzania imekubali ombi la serikali ya Kenya, kupeleka madaktari 500 kwenda kutoa huduma Kenya. Hii ni fursa kwa madaktari mmoja mmoja. Lakini sio fursa kwa serikali ambayo wajibu wake wa kikatiba ni kutoa huduma za afya kwa wananchi wake. Hivyo, serikali inapoteza nguvu kazi muhimu ambayo ingeweza kuisadia kutimiza wajibu wake.

Zaidi, serikali inasema kwamba nchi itanufaika kwa madaktari wake wasiokuwa na ajira kwenda Kenya kupata uzoefu. Je, ni uzoefu wa kutibu ugonjwa gani ambao hapa nchini hatuwezi kuutibu na kwamba Kenya wana uzoefu mkubwa kutuzidi? Je, serikali itaingia makubaliano na hao madaktari wanaokwenda Kenya kwamba wakirudi watapangiwa hospitali ili kutumia huo uzoefu waliokwenda kujifunza?

Serikali kwa upande wake imekiri kuna madaktari 1,764 waliomaliza mafunzo kwa vitendo ambao hawajapata ajira. Madaktari wasio na ajira wana haki ya kujipatia kipato na kuendeleza taaluma zao, hivyo tunaamini ni haki yao kama binadamu huru kutafuta kazi popote nchini au nje ya nchi kuliko kukaa bure. Mazingira ya upatikanaji na usalama wa ajira hutengenezwa na serikali, iwe katika sekta za umma au binafsi.

Ongezeko la uzalishaji wa madaktari na wataalamu wengine wa afya tunaloshuhudia leo ni matokeo ya sera na mipango ya serikali. Kwa mfano, udahili wa wanafunzi uliongezeka kutoka 1,013 mwaka 2005 hadi kufikia 4,147 mwaka 2009. Hii ilitokana na mipango ya serikali kuwezesha vyuo vya mafunzo vya umma na binafsi kifedha, kisera na kitaalamu. Mpango huu bado unaendelea.

Sambamba na kuongeza udahili na uzalishaji wa wataalamu, serikali iliongeza pia nafasi za ajira. Wataalamu walimaliza mafunzo na kupangiwa moja kwa moja kwenye vituo vya kazi. Lakini, tatizo tulilionalo leo ni kwamba uzalishaji wa wataalamu umeendelea kuongezeka wakati ajira zimesitishwa.

Ni lazima kila mwaka kuajiri madaktari wapya kwa sababu waliopo pia hupungua kwa sababu mbalimbali. Kuna wanaopatwa na maradhi hivyo kushindwa kutekeleza majukumu yao, wapo wanaobadilisha fani na kufanya shughuli zingine, wanaostaafu, wanaohama nchi, wanaofariki, na wanaopunguza ufanisi kwa sababu mbalimbali.

Kwa hiyo, iwapo serikali kupitia tamko lake la tarehe 21/03/2017 inasema kwamba haijaajiri madaktari wapya tangu 2014 inatia shaka kama hiyo idadi wanayosema wapo wanatoa huduma ndiyo idadi halisi. Lakini pia tamko hilo la serikali tunalichukulia kama tangazo rasmi kwamba haina uwezo wa kuajiri madaktari wote wanaofuzu kila mwaka.


Hii ina maana kwamba serikali imekwepa wajibu wake wa msingi wa kuhakikisha wananchi wanapata huduma bora kupitia wataalamu waliofuzu. Ni ishara ya kukiri kushindwa; kama hospitali na vituo vya kutolea huduma za afya vya umma vinahitaji jumla ya madaktari 3,460 lakini tunao 1,764 wasio na ajira na bado tuko radhi kuwapeleka Kenya!

Kwa maoni yetu, tunahitaji kufanya mambo mawili kwa kasi na umakini mkubwa. Jambo la kwanza, tunashauri serikali ipanue wigo wa sekta binafsi katika kutoa huduma za afya. Hii inatokana na serikali kukiri haina uwezo wa kuajiri wataalamu wote wanaozalishwa kila mwaka. Hospitali binafsi zikiwezesha na kuwekewa

mazingira bora ya kujiendesha zitaajiri zaidi hivyo kuwezesha wananchi wengi zaidi kupata huduma.

Pili, serikali ipeleke mswada wa bima ya afya kwa kila mtanzania Bungeni haraka iwezekanavyo. Bima kwa kila mtanzania ni muhimu ili kuwezesha wananchi kumudu gharama za huduma kwenye hospitali binafsi na za umma. Pia bima itawezesha hospitali kujipatika mapato na kujiendesha hivyo kupunguza mzigo kwa serikali katika kugharamia huduma za afya kwa wananchi.

Angalizo la msingi kwa serikali ni kuongeza usimamizi, udhibiti na uratibu wa ubora wa huduma za afya kwa vituo vya umma na binafsi pamoja na kuweka sera shirikishi na rafiki kwa taasisi zote zinazotoa huduma za afya nchini.



Mr. Irenei Kiria

Executive Director of Sikika,

P.O. Box 12183 Dar es Salaam,

Tel: +255 222 666355/57, Fax: 2668015, Email: [info@sikika.or.tz](mailto:info@sikika.or.tz), Website: [www.sikika.or.tz](http://www.sikika.or.tz)